

# Mauguzi ya Maambukizo ya Kifua Kikuu Kilichojiika


Ukaguzi wako unaonyesha kuwa una Kifua Kikuu kilichojiika, au “LTBI.” Mtu akiwa na LTBI viini vya Kifua Kikuu katika mwili wao huwa “vimelala” lakini bado viko hai. Viini vya Kifua Kikuu “vitalala” bora tu mwili wako uweze kuendelea kukabiliana navyo. Ukiwa na LTBI hauwezi kuambukiza wenzako Kifua Kikuu.

Mwili wako ukiwacha kukabiliana na viini vya Kifua Kikuu, “vitaamka” na kuanza kukuwa.

**Jambo hili linaweza kumfika mtu yeyote mwenye LTBI wakati wowote.** Viini vikikuwa na kuenea huitwa “ugonjwa wa Kifua Kikuu stawi.” Watu wenye ugonjwa wa Kifua Kikuu stawi waweza kuwa wagonjwa sana na kueneza Kifua Kikuu kwa wenzao.

## Nawezaje kuzuia ugonjwa wa Kifua Kikuu stawi?

Isoniazid (INH) ni dawa ya kawaida inayotumika kuuguzi LTBI. INH huuwa viini “vilivyolala” vya Kifua Kikuu **kabla** havijapata nafasi ya kukufanya uwe mgonjwa. Kwa sababu viini vya Kifua Kikuu vina nguvu, dawa huchukuwa miezi mingi kuvizuia.



INH hufanya kazi vyema zaidi ukiitumia kila siku hadi daktari wako anaposema ni sawa uache kuitumia.

Unatakiwa umuone daktari wako mara moja kwa mwezi unapoendelea kutumia INH ili uhakikishe mauguzi yako yanaendelea vyema.

## Kwanini nitumie dawa kama sijisikii mgonjwa?

INH huuwa viini vya Kifua Kikuu mwilini mwako **kabla** havijapata nafasi ya “kuamka” na kukufanya mgonjwa.

## Nafaa kufahamu nini kuhusu dawa ya LTBI?

Watu wengi hutumia INH kila siku bila matatizo yoyote, lakini **watakiwa ujihadhari na mambo kadhaa:**

- Homa ya zaidi ya siku tatu
- Kukosa hamu ya chakula, kukonda, aukujisikia mchofu bila sababu
- Kizunguzungu au kutapika:
- Maumivu ya tumbo
- Mkojo wa rangi nzito (kama chai au kahawa)
- Ngozi au macho ya rangi ya manjano
- Upele au kuwashwa ngozi
- Kufa ganzi au kuwashwa Mikono au miguu
- Kukohowa kwa zaidi ya wiki tatu
- Kutoka jasho usiku

**Ukiwa na yoyota kati ya matatizo haya, wacha kutumia INH na upigie simu zahanati yako mara moja – usingojee miadi yako ijayo.**

## Mambo mengine muhimu:

- **Kunywa tembo** anapotumia INH kwaweza kudhuru maini yako. Usinywe tembo, mvinyo hadi umalize mauguzi yako ya LTBI.
- Mwambie daktari wako kama watumia **dawa nyengine** au una **mimba**.



## Mauguzi ya Maambukizo ya Kifua Kikuu Kilichojojificha – ukurasa wa 2

### Itakuwaje nisipotumia dawa?

Usipotumia INH au ukiwacha kutumia vidonge kabla wakati, waweza kuwa mgonjwa na uugue ugonjwa wa Kifua Kikuu stawi. Hali hii yaweza kumfika **mtu yeyote** mwenye LTBI **wakati wowote**.

### Nifanyeje nikiwa nimepata chanjo ya BCG?

Katika nchi ambapo Kifua Kikuu huweko kwa kawaida, watu wengi hupata chanjo iitwayo BCG. BCG yawezakulinda watoto wasipate Kifua Kikuu, lakini hudumu miaka michache tu.

Watu waliopata BCG wanawezakupata ugonjwa wa Kifua Kikuu stawi! Kama umepata BCG, bado wawezakujilinda kwa kutumia dawa dhidi ya LTBI.

### Je nikihama?

Ukihamia jimbo au mji mwengine, mueleze mhudumu wako wa afya **kabla haujahama**. Wanaweza kuhakikishia unapata dawa zako za Kifua Kikuu baada ya kuhama.

**Jilinde pamoja na jamii yako, na marafiki kutokana na Kifua Kikuu – Tumia dawa zako zote za Kifua Kikuu!**

### Nitakumbuka vipi kutumia dawa zangu za Kifua kikuu?

**Ni muhimu sana utumie INH yako kila siku.** Ikipita siku nyingi kabla haujatumia dawa huenda isifanye kazi. Endelea kuitumia hadi daktari wako aseme ni sawa usiendeleo kuitumia.

Mambo kadhaa yaweza kukusaidia kukumbuka:

- Weka vidonge vyako mahali ambapo utaziona kila siku.
- Mwambie mtu katika jamii yako au rafiki akukumbushe.
- Weka alama katika kalenda kila siku baada ya kutumia vidonge.
- Tumia kisanduku cha vidonge.
- Tumia dawa yako kidonge saa ile ile kila siku. Kwa mfano, baada ya kupiga mswaki, chakula cha asubuhi, au kabla tu ya kalala.

Ukikosa kuitumia siku zozote, andika siku hizo ndio uweze kumwambia daktari au muuguzi wako wakati utakapoonana nao tena.

### Zahanati yako:

---



---



---

Simu #: \_\_\_\_\_